



Kamwe, hatoingia motoni mtu yeyote aliyeswali kabla ya kuchomoza Jua na kabla ya kuzama kwake

Kutoka kwa Abuu Zuhairi Umara bin Ruaiba radhi za Allah ziwe juu yake amesema:
Amesema Mtume rehema na amani ziwe juu yake: "Kamwe, hatoingia motoni mtu
yeyote aliyeswali kabla ya kuchomoza Jua na kabla ya kuzama kwake"

[Sahih] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Anaeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake: Kuwa hatoingia motoni mtu yeyote
aliyeswali swala ya Alfajiri, na swala ya Lasiri, na akadumu nazo; na amezitaja maalumu
swala hizi mbili; kwa sababu ndizo swala nzito zaidi, na kwa sababu wakati wa Alfajiri huwa ni
wakati wa usingizi na ladha yake, na wakati wa Lasiri huwa ni wakati wa kushughulishwa na
kazi za mchana na biashara zake, na atakayezihifadhi swala hizi mbili pamoja na kupatikana
tabu ndani yake, basi bila shaka atawea kuzihifadhi swala zingine zilizobakia.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/6215>

